# OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

## HOTUBA

## YA

## MHE. HAMZA S. JOHARI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA SHERIA TANZANIA

## VIWANJA VYA CHINANGALI - DODOMA

## 3 FEBRUARI, 2025

- **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**
- **Mhe. Profesa Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania,**
- **Mhe. Khamis Ramadhani Abdallah, Jaji Mkuu wa Zanzibar,**
- **Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**
- **Mhe. William Vangimembe Lukuvi (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu),**
- **Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria;**
- **Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri mliopo,**
- **Wahe. Majaji wa Mahakama ya Rufani mliopo,**
- **Mhe. Mustapher M. Siyani, Jaji Kiongozi Mahakama Kuu ya Tanzania,**
- **Mhe. Juliana Masabo, Jaji Mfawidhi, Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma,**
- **Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu mliopo,**
- **Wahe. Majaji Wastaafu wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu mliopo,**
- **Mhe. Rosemary Staki Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma,**

- **Bw. Emmanuel Tutuba, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania,**
- **Mhe. Eva Kiaki Nkya, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania,**
- **Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama,**
- **Bw. Baraka Leonard, Katibu wa Bunge,**
- **Waheshimiwa Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wote mliopo,**
- **Mheshimiwa George Hillary Herbert, Msajili Mahakama ya Rufani,**
- **Bw. Sylvester Anthony Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka,**
- **Dkt. Ally Possi, Wakili Mkuu wa Serikali,**
- **Bw. Amedeus Shayo, Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania (TPBA),**
- **Wakili Boniphace Anyisile Kajunjumele Mwabukusi, Rais wa Chama cha Mawakili wa Kujitegemea (TLS),**
- **Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Taasisi na Mashirika ya Kimataifa,**
- **Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa sasa na Wastaafu mliopo,**
- **Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Kitaaluma, Siasa na Dini mliopo,**

- **Waheshimiwa Wasajili na Naibu Wasajili,**
- **Waheshimiwa Mahakimu,**
- **Watendaji na Watumishi wa Mahakama mliopo,**
- **Mawakili wa Serikali na Mawakili wa Kujitegemea,**
- **Watoa huduma za sheria wote mliopo,**
- **Ndugu wanahabari,**
- **Wageni waalikwa, na**
- **Mabibi na Mabwana.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA ...**

**Mheshimiwa Rais**,

Ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia afya njema ya kuweza kukutana hapa leo ili kushiriki kilele cha maadhimisho ya Siku ya Sheria Tanzania. Kwa namna ya pekee nitumie nafasi hii kukupongeza kwa kuingoza nchi yetu kwa uzalendo wa hali ya juu. Ninakushukuru sana kwa kuniteua na kuendelea kuniamini kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ninaahidi nitatekeleza majukumu yangu kwa uaminifu.

**Mheshimiwa Rais**,

Maadhimisho ya Siku ya Sheria Tanzania nchini yana malengo matatu. Mosi, ni kuashiria kuanza kwa mwaka wa Mahakama, Pili ni kutathmini

dhana ya utoaji haki na mchango wa kila taasisi inayotoa haki. Tatu, ni kuwaombea Majaji na Mahakimu ili watekeleze majukumu yao ya kutenda haki kwa hekima na busara.

**Mheshimiwa Rais**,

Kauli mbiu ya Maadhimisho ya Siku ya Sheria Tanzania kwa mwaka huu ni: “***Tanzania ya 2050: Nafasi ya Taasisi zinazosimamia haki madai katika kufikia malengo makuu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo”.*** Kauli mbiu hiyo inatutaka tueleze namna ambavyo taasisi zinazosimamia haki madai zinatekeleza au zinajipanga kutekeleza malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

**Mheshimiwa Rais**,

Kabla sijaeleza namna ambavyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inatekeleza malengo yaliyoainishwa katika Rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ni vema tufahamu kuwa, zipo taasisi nyingi zinazosimamia haki madai ambazo kazi yake ni kushughulikia huduma za haki zinazowahusu ama mwananchi mmoja mmoja, kikundi cha watu, kampuni au taasisi ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mahakama, kutaja kwa uchache. Ngazi ya taasisi hizi katika kusimamia haki inaweza kuwa ile ya kiwango wianishi au rekebishi kama ambavyo

mwanafalsafa ***Aristotle*** aliwahi kuzigawa haki hizo na kuziita **"*distributive* and *corrective justice*".**

**Mheshimiwa Rais**,

Dhana ya ***distributive and corrective justice*** inajitokeza pale ambapo taasisi zote zinazohusika na utoaji haki zinatenda haki na mnufaika wa kwanza anakuwa ni mwanachi au kundi la wananchi, wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na hatimaye taifa kwa ujumla. Utendaji haki huo kwa lugha rahisi ni kuridhishwa kwa huduma itolewayo kwa kuzingatia misingi ya ubora, weledi na ufanisi. Hii ndiyo maana ya haki wianishi ***(distributive justice)***. Pale ambapo mwananchi au kundi la wananchi halijalizika na maamuzi ya taasisi inayopaswa kutoa haki wianishi ambayo imebainishwa kisheria na mwananchi huyo au kundi la wananchi wakaamua kwenda kutafuta haki katika chombo cha juu chenye kauli ya mwisho juu ya haki kwa mujibu wa Katiba na sheria za nchi yaani Mahakama ili kupata msimamo wa nani alikosea wapi na aliyekosewa anastahili nini, kwa mujibu wa mwanafalsafa ***Aristotle*** haki hii huitwa haki rekebishi ***(Corrective Justice)***.

**Mheshimiwa Rais**,

Nimepata fursa ya kushiriki katika vikao mbalimbali vya kujadili Rasimu ya Dira na kupitia kwa kina Rasimu hiyo na kubaini kuwa, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ni mojawapo ya nyenzo muhimu sana ambayo inapaswa izingatiwe na taasisi zinazosimamia haki madai kwa mustakabali wa Taifa letu. Katika safari yetu ya kuelekea Tanzania ya 2050, taasisi zinazohusika na usimamizi wa haki madai ni muhimu zikajikita katika kutekeleza malengo yaliyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kwa kuifanya Tanzania kuwa ni nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu yenye uchumi mseto, stahimilivu, imara na jumuishi; kutokomeza umaskini, kuimarisha maisha na ustawi kwa watu wote, kuwajengea uwezo wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kuwa na mfumo wa utawala wenye uwazi, uwajibikaji, kuimarisha amani, uhuru na usalama wa watu na kuhakikisha usimamizi thabiti na endelevu wa rasilimali zetu.

**Mheshimiwa Rais**,

Malengo Makuu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 yanaweza kufikiwa ikiwa kila raia atapata haki yake bila vikwazo vya aina yoyote kutoka katika taasisi husika inayosimamia haki madai, kutakuwa na mifumo imara ya kisheria na kitaasisi itakayowezesha haki kufikiwa kwa haraka na kwa ufanisi na kila taasisi inayosimamia haki madai itafanya tathmini ya

mipango na mikakati yake ili kuona kama inaendana na kasi ya viwango, ubora, ufanisi na tija inayolengwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

**Mheshimiwa Rais**,

Tunatambua kuwa, Tanzania inajivunia historia kubwa ya amani, mshikamano na umoja ambao umekuwa nguzo muhimu katika kufanikisha Dira ya Maendeleo inayoisha mwaka 2025. Katika muktadha huu, tunapojiandaa kuelekea mwaka 2050 ni muhimu kuzingatia nafasi ya haki, utawala wa sheria na utawala bora kama mihimili mikuu ya mafanikio yetu. Haki, ustawi na maendeleo ya wananchi wetu vinategemea pia misingi imara ya sheria na taasisi zinazosimamia haki madai.

**Mheshimiwa Rais**,

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikiwa ni miongoni mwa taasisi zinazosimamia haki madai ina nafasi kubwa ya kufikia malengo yaliyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050. Hili linajidhihirisha katika Mpango Mkakati wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2025/2026 ambao umeainisha vipaumbele vya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kila mwaka wa fedha ili kuhakikisha kila kinachofanyika katika ofisi hii kinachangia kwa namna moja au nyingine kuharakisha matokeo yanayokusudiwa katika Dira

ya Taifa ya Maendeleo 2050. Sambamba na hilo, Dira ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inalenga kuifanya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ***kuwa Taasisi yenye ufanisi, kitaaluma na kuaminika katika kutoa huduma bora za kisheria kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***. Kadhalika, dhima ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni ***kutoa huduma za kisheria zenye ubora kwa njia ya kuandaa Sheria, Upekuzi na Majadiliano ya Mikataba pamoja na Ushauri wa Kisheria kwa Maendeleo ya Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa***. Azma yetu ni kuhakikisha watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi, weledi, ubora na uwajibikaji. Hivyo basi, tutahakikisha tunaimarisha uwezo wa kitaasisi na kuwajengea uwezo thabiti wanasheria wetu kupitia mafunzo mbalimbali kuendana na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

**Mheshimiwa Rais**,

Kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni jukumu langu kuhakikisha natoa ushauri wa kisheria ambao utaisaidia Serikali na taasisi zinazosimamia haki madai kutunga sheria zenye maslahi kwa Serikali na Taifa kwa ujumla. Katika kutekeleza jukumu hilo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itapitia sheria zote zilizopitwa na wakati ili ziendane na mazingira halisi ya Tanzania ya 2050 kwa kukuza uchumi katika nyanja za kodi, manunuzi,

ubunifu, teknolojia, masoko ya mitaji na fedha. Nitoe rai kwa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kufanya utafiti wa kina kabla ya kutunga sheria ili Sheria zitakazotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ziendane na maendeleo ya sayansi na teknolojia kama inavyolengwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Wakati huo huo, zoezi la kutafsiri sheria kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza ili ziweze kukidhi mahitaji ya watumiaji linaendelea. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Disemba, 2024 Sheria Kuu **300** zilifanyiwa ufasiri kutoka lugha ya kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili.

**Mheshimiwa Rais**,

Katika jitihada za kuhakikisha Malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 yanafikiwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kuwahimiza Mawakili wa Serikali na Wanasheria wote walio katika utumishi wa umma kujiendeleza na kushiriki mafunzo ya fani mbalimbali na sio fani ya sheria tu ili waweze kufanya upekuzi wa Mikataba na Hati za Makubaliano kwa ufanisi na ufasaha. Mafunzo yatakayotolewa yatawapatia maarifa shindani ya kitaifa na kimataifa na kuwafanya washiriki na kutoa mchango thabiti katika majadiliano ya kimkataba na migogoro mbalimbali inayoihusu Serikali ndani na nje ya nchi ili kulinda rasilimali zetu. Kati ya mwezi Julai hadi Disemba, 2024 jumla ya Mikataba ya Kitaifa, Kikanda na

Kimataifa **1,799** na Hati za Makubaliano (Memoranda of Understanding) **352** zilifanyiwa upekuzi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Thamani ya Mikataba hiyo ni kubwa sana na imesaidia kuongeza ukuaji wa pato la taifa na kuvutia uwekezaji nchini.

**Mheshimiwa Rais**,

Kwa kuwa teknolojia ina nafasi kubwa katika kuifikia Tanzania ya 2050, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma za kisheria kwa kuweka mifumo madhubuti ya TEHAMA na kuweka msisitizo kwa Mawakili wa Serikali nchini kuendelea kujisajili na kuweka taarifa zao katika Rejesta ya Mfumo wa Taarifa za Mawakili (Office of Attorney General – Management Information System - OAG-MIS) ambao uliuzindua tarehe 29 Septemba, 2022 katika Mkutano wa Chama cha Mawakili wa Serikali ulifanyika hapa jijini Dodoma. Yote haya yanatarajia kuongeza ufanisi na kupunguza ucheleweshaji wa huduma zetu za sheria. Njia hii pia itaongeza uwazi na uwajibikaji katika mfumo wa utoaji haki madai.

**Mheshimiwa Rais**,

Tumeshuhudia katika miaka ya hivi karibuni jinsi mahakama ya Tanzania ilivyopiga hatua katika kuboresha utoaji haki kwa kusogeza huduma karibu

na wananchi kwa kujenga vituo jumuishi vya utoaji haki, kujikita katika matumizi ya TEHAMA katika kutoa haki na kupunguza hatua za kusikiliza mashauri ya madai kutoka hatua 38 mpaka kufikia 21. Suala hili ni mchango mkubwa katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kwa sababu linachangia kuvutia biashara na uwekezaji hapa nchini. Ni katika misingi hiyo hiyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kutafuta fedha za Kuendeleza ujenzi wa Vituo Jumuishi vya Taasisi za Kisheria *(Government Legal Institutions Integrated Centers-GLIICs)* katika Mkoa wa Mwanza na Arusha. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2024 ujenzi wa jengo la Arusha umefikia **45%** na Mwanza **64%**. Ujenzi wa majengo haya ukikamilika utasogeza huduma karibu na wananchi na utasaidia utekelezaji wa majukumu ya taasisi zetu kwa mujibu wa Katiba na sheria, kurahisisha utendaji kazi, kupunguza gharama za uendeshaji wa ofisi, kutoa haki kwa wakati na kuondoa migongano ya maslahi na wadau mbalimbali.

**Mheshimiwa Rais**,

Tarehe 9 Disemba, 2023 wakati unafungua Mkutano wa Kwanza wa Kitaifa wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 jijini Dodoma ulisema kuwa ***"... suala la kuwa na Dira ya Taifa, sio tena utashi wa Rais aliyepo madarakani wakati huo, bali ni suala la kisheria".*** Kwa mantiki hiyo, taasisi zinazosimamia haki madai zinapaswa kufahamu kuwa utekelezaji wa

malengo makuu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ni takwa la kisheria. Hivyo, taasisi hizo zinapaswa kuwa na uwezo, uhuru na rasilimali za kutosha ili kutoa huduma bora kwa wananchi kazi ambayo ninafurahi kusema kuwa chini ya usimamizi wa Serikali yako zinaendelea kufanyika vizuri.

**Mheshimiwa Rais**,

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kushirikiana kwa karibu na taasisi zinazohusika na haki madai pamoja na wadau wengine kama Mahakama, asasi za kiraia, mashirika ya kimataifa na jumuiya za kikanda na kimataifa ili kuboresha utawala wa sheria na haki katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Sambamba na hilo napendekeza, mfumo wa uendeshaji wa Mabaraza ya Kodi, Ardhi, Tume ya Ushindani, Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA) na taasisi nyingine za udhibiti ufanyiwe maboresho ili kukabiliana na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

**Mheshimiwa Rais**,

Ni matumaini yangu kuwa, Tanzania ya 2050 itakuwa ni taifa lenye mafanikio na maendeleo endelevu iwapo kutakuwa na taasisi imara zinazohusiana na haki madai na usimamizi wa sheria. Ninaamini kuwa,

kupitia ushirikiano wa wananchi na taasisi zinazohusika na haki madai tutapata mafanikio makubwa katika kufikia malengo yetu ya maendeleo. Hakika, mfumo wa haki utakuwa nguzo muhimu katika kufikia Tanzania yenye ustawi, usawa, na maendeleo kwa kila raia.

**Mheshimiwa Rais;**

Baada ya kusema hayo, nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa kupata nafasi hii ya kutoa salamu pamoja na hotuba yangu katika maadhimisho haya yanayoashiria ufunguzi wa shughuli za Mahakama hapa nchini. Aidha, kwa kuwa leo ni mara ya kwanza kukutana na wengi wenu mliopo hapa kwa mwaka huu, naomba nimalizie hotuba yangu kwa kuwatakia watanzania na wadau wote wa sheria na haki heri na fanaka kwa mwaka 2025.

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**